# KATIBA YA UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA (TANZANIA COMMITTEE CLERK'S UNION)

# TACCU

NOVEMBER 26, 2023

**URATIBU NA USIMAMIZI BORA WA VIKAO NA MIKUTANO NI NGUZO YA UTAWALA BORA KATIKA MAMLAKA ZA UMMA**

REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

# KATIBA YA UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA

# (TANZANIA COMMITTEE CLERK's UNION)-"TACCU"

## *UTANGULIZI.*

I. Lengo la umoja huu ni kukuza na kudumisha kada hii, uwajibikaji na hadhi ya kada ya Katibu wa Kamati (Committee Clerk "CC") kwa kuhamasisha na kuwasaidia wanachama kuendeleza fani zao ndani na nje ya mipaka ya kada ya Katibu wa Kamati (Committee Clerk "CC"); na

II. Lengo letu ni kuwakilisha Makatibu wa kada ya Katibu wa Kamati (Committee Clerk "CC"), Kitaifa na kimataifa kwa kudumisha na kuimarisha mawasiliano na mahusiano mazuri miongoni mwa wanakada wa Katibu wa Kamati (Committee Clerk "CC"); na

III. Malengo mengine ni kuwa na muongozo mmoja unaoitambua kada hii ya makatibu wa kamati, masuala ya kusaidiana wakati wa shida pamoja na kuwa na chombo cha kuiwakilisha jamii ya wana kada hii katika mamlaka mbali mbali. Pia umoja umeanzishwa ili kupata nguvu ya kisheria katika kuendesha na kusimamia shughuli za kila siku za umoja kwa mujibu wa kanuni na taratibu za rasimu ya katiba itakayo ongoza umoja huu bila kuathili miongozo mbali mbali inayotolewa na mamlaka za serikali na serikali za mitaa.

IV. Katibu wa Kamati (Committee Clerk "CC") kama raia mwingine yeyote nchini ana haki ya kupata huduma bora za kijamii, kiuchumi na kimaslahi kama vile Afya, Elimu, Chakula, Malazi, Usafiri na huduma nyingine za kijamii;

V. Hivyo, Sisi Makatibu wa Kamati (Committee Clerk "CC") wote kwa pamoja, tunaazimia kuungana na kuunda umoja wetu utakaohakikisha kuwa, tunatekeleza wajibu wetu kwa kutoa huduma bora kwa mamlaka za umma ambazo ndizo waajiri wetu, kuweka mazingira na mahusiano baina ya wajiri na watumishi kuhusu kukuza kada ya Katibu wa Kamati (Committee Clerk "CC") wanachama, kuboresha na kuendeleza maslahi ya Katibu wa Kamati (Committee Clerk "CC") wanachama bila kujali tofauti za sekta au maeneo Mwanachama anapotoka.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

## SEHEMU YA KWANZA

### *1.1 TAFSIRI NA UFAFANUZI*

Labda kama itaelezwa vinginevyo, maneno yatakayotumika katika Katiba hii yatakuwa na maana halisi kwa mujibu wa Katiba ya Umoja wa "TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION" kama ifuatavyo:

1.2 **Umoja-** maana yake ni muungano wa wanachama waliojiunga kwa hiari na kukubaliana na kanuni, taratibu na mashariti ya katiba hii

1.3 **Mkutano mkuu-** maana yake ni muundo wa kikao cha juu cha kupitisha maamuzi kuhusu shughuli mbalimbali za Umoja wa "TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION".

1.4 **Kamati Tendaji-** maana yake ni chombo cha ngazi ya juu kitakacho jishughulisha na masuala ya utawala, uendeshaji, usimamizi na uratibu wa shughuli za umoja za kila siku ambayo itakuwa na wajumbe saba (7).

1.5 **Kanuni** maana yake ni sheria ndogo zilizotungwa na wanachama ili kuhakikisha kunakuwepo na uendeshaji na usimamizi mzuri wa Umoja wa "TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION" bila kuathili katiba ya umoja huu.

1.6 **Masuala mtambuka** ni mambo yale yote ambayo serikali na jamii inapaswa kuyatilia maanani katika kuyaishi nayo. Masuala hayo nikama vile, Mazingira, UKIMWI, Jinsia, Rushwa, makundi yenye mahitaji maalumu,

**1.7 Mamlaka za Umma** kwa mujibu wa katiba hii, mamlaka za umma zitajumuisha mmlaka zote zinazotoa huduma kwa jamii za kiutawala, kiuongozi, kiusimamizi, na zile zinazo fanana na huduma hizi. Mamlaka hizo zitajumuisha Halmashauri za Wilaya, Halmashauri za Miji, Halmashauri za Majiji, Halmashauri za Manispaa, wakala wa serikali, Mashirika ya Umma, Makampuni binafsi na yale ya Umma

**1.8 Committee Clerk (CC)** ni katibu wa kamati kwa mujibu wa Muongozo wa Utumishi wa Umma, ambapo inamaanisha ni yule mtumishi ambaye anafanya kazi za Kuratibu taratibu za mikutano na vikao, kuandaa mihtasari ya vikao na Mikutano, kufuatilia utekelezaji wa maagizo (maazimio) yaliyo fikiwa katika vikao, pamoja na kufanya maandalizi yote yanayowezesha kufanikisha kikao au mkutano katika mamlaka za umma bila kusahau maandalizi ya stahiki za wajumbe wa vikao/mikutano husika.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

## SEHEMU YA PILI

### *2.1 JINA, MAKAO MAKUU, ANUANI NA USIMAMIZI WA UMOJA*

Labda kama itaamuliwa vinginevyo, jina, makao makuu, anuani na usimamizi wa Umoja utakuwa kama ifuatavyo:

### *2.2 JINA LA UMOJA*

Umoja huu utajulikana na kuitwa kwa jina la Kiswahili **UMOJA WA MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA** na kwa kiingereza **"TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION"**

### *2.3 MAKAO MAKUU YA UMOJA.*

Makao makuu ya umoja huu yatakuwa Mkoa wa Dodoma, Kata ya Makole -Tanzania.

### *2.4 ANUANI YA UMOJA*

Anuani ya Umoja huu ni Umoja wa "TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION", S. L. P 1551 DODOMA, TANZANIA.

### *2.5 ENEO LA UMOJA.*

Umoja huu utafanya kazi katika Jamuhuri ya muungano wa Tanzania na utajumuisha Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

### *2.5 ENEO LA SHUGHULI ZA UMOJA.*

Shughuli za Umoja wa "TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION" zitafanyika katika Jamuhuri ya muungano wa Tanzania na utajumuisha Tanzania bara na Tanzania visiwani.

## SEHEMU YA TATU

### *2.0 MALENGO*

1) Kuwa na umoja wa kudumu ambao unalenga kuboresha kada husika na kuiwezesha kada ya makatibu wa kamati kuthaminiwa mahala pa kazi.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

2) Kufanya umoja kuwa njia rahisi ya kusimamia, kutunza, na kupata ushauri wa namna ya kuboresha utendaji kazi ili kuleta tija na ufanisi zaidi wa kada hii.
3) Kujenga na kuimarisha ushirikiano na mawasiliano miongoni mwa wana kada wa kada hii na kada zingine zinazofanya kazi katika mamlaka za umma.
4) Kuwa kiungo cha msingi kati ya umoja na taasisi mbalimbali za umma.
5) Kuwa mahala pa kubadilishana uzoefu miongoni mwa wanachama wa Umoja wa MAKATIBU WA KAMATI TANZANIA, "TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION " na taasisi nyingine za ndani na nje ya nchi.
6) Kusaidia jamii ya wanachama na jamii inayotuzunguka katika kutatua matatizo muhimu ya kijamii ikiwemo ujinga, maradhi, umaskini, malazi na ukosefu wa chakula bila kusahau masuala mtambuka.
7) Umoja utaweza kufanya shughuli zingine za maendeleo zisizo na faida na zile zenye muelekeo wa faida kwa njia ya kushirikiana na wafadhili wa miradi mbalimbali waliopo ndani na nje ya nchi kwa lengo la kusaidia na kuboresha Maisha ya wanachama pamoja na jamii inayo zunguka bila kuathili utendaji kazi wa mamlaka husika ambazo ni waajiri.

## SEHEMU YA NNE

### *4.1 MWANACHAMA*

Kutakuwa na wanachama wa aina mbili kama ifuatavyo:

#### MWANACHAMA MWANZILISHI

Mwanachama mwanzilishi wa Umoja ni yule aliyeshiriki kikamilifu katika hatua zote za awali za uanzishaji wa umoja huu.

#### MWANACHAMA WA KAWAIDA

Ni mwanachama yeyote ambaye si mwanzilishi, lakini amejiunga na umoja huu baada ya kutimiza masharti ya kujiunga kama yalivyowekwa katika katiba hii ya umoja pamoja na kanuni zake.

#### SIFA ZA MWANACHAMA

a) Awe na umri usiopungua miaka 18
b) Awe mwaminifu na akubalike na wenzake
c) Awe mfanyakazi wa kada ya katibu wa kamati (CC) katika malaka za umma.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

d) Akubali na kuheshimu katiba na Kanuni za umoja
e) Awe na akili timamu
f) Awe tayari kulinda, kusimamia na kutetea umoja katika Nyanja mbalimbali wakati wote.
g) Akubali kukosolewa pale anapokosea
h) Awe raia wa Tanzania asiye na kikwazo cha uraia wake
i) Awe amelipa michango yote inayotakiwa ndani ya umoja kwa mujibu wa katiba ya umoja.
j) Awe mtumishi wa kada hii ambaye anafanya kazi katika Jamuhuri ya muungano wa Tanzania

### 4.1.4 UTARATIBU WA KUJIUNGA NA UMOJA KWA WANACHAMA WAPYA

a) Mwombaji ataandika barua ya maombi ya kujiunga na umoja kwa Mwenyekiti, na umoja utajadiliwa.
b) Maombi yanaweza kukubaliwa au kukataliwa kulingana na sifa za mwombaji na sababu zingine
c) Mwombaji aliyekubaliwa au kukataliwa atapewa taarifa.
d) Muombaji aliyekubaliwa atachangia michango kama itakavyoamuliwa:

## *4.2 KUKOMA KWA MWANACHAMA.*

Mwanachama atakoma kutokana na sababu zifuatazo:

1) Kuhama Tanzania ambako kutasababisha kukatika kwa mawasiliano kati yake na wanaumoja wa umoja wa "TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION" pamoja na uongozi kwa ujumla.
2) Kifo cha Mwanaumoja mwenyewe.
3) Kufukuzwa uanachama kutokana na ukorofi au utovu wa nidhamu baada ya kuthibitishwa na kuidhinishwa na mkutano mkuu.
4) Mwanachama kupatwa na ugonjwa wa akili, utakaothibitishwa na daktari.
5) Kufanya mambo ambayo ni kinyume cha maadili au kuidharirisha katiba ya Umoja.
6) Kwa kukiuka katiba inayoongoza umoja huu.
7) Kutoshiriki shughuli za Umoja mara tatu mfululilzo bila taarifa yoyote;;

## *4.3 WAJIBU WA MWANACHAMA*

1) Kushiriki kikamilifu katika shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Umoja.
2) Kutoa na kuwasilisha michango kwa kiwango kitakachoamuriwa na Mkutano Mkuu.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

3) Kuhudhuria vikao vyote ambavyo yeye ni mjumbe.
4) Kubeba dhamana endapo janga litakumba Umoja.
5) Kuilinda na kuitetea katiba ya Umoja.

### *4.4 HAKI ZA MWANACHAMA*

Kila mwanachama atakuwa na haki zifuatazo: -

a) Kutoa mchango wake wa mawazo pamoja na kusikilizwa katika vikao vya Umoja.
b) Kupiga kura katika kutoa maamuzi ili kukidhi matakwa ya kuendesha Umoja
c) Kupata taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Umoja.
d) Kugombea nafasi ya uongozi katika wadhifa wowote kwenye chaguzi za Umoja.
e) Kupata huduma za kijamii toka kwenye umoja pale ambapo itaruhusu.
f) Kushiriki semina, mafunzo

### *4.5 MAMBO YA KUZINGATIA*

Ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo kwa maslahi ya Umoja; -

1) Mwana kada yeyote wa kada hii ya makatibu wa kamati ambaye sio mwana umoja mwanzilishi, akitaka kuwa mwana umoja ataleta maombi kimaandishi kwa mwenyekiti wa umoja.
2) Mwombaji aliyekubaliwa kujiunga na Umoja atajulishwa kukubaliwa kwake na atalipa ada ya kiingilio pamoja na michango kama itakavyokuwa imeamuliwa na mkutano mkuu wa mwaka.
3) Umoja utakuwa na daftari la wana umoja lenye maelezo muhimu ya kila Mwana umoja.
4) Mwana umoja ambaye uanachama wake umekoma, hatarudishiwa kiingilio isipokuwa michango yake ambayo utaratibu utakuwa umeainishwa katika kanunu zinazoongoza taratibu za fedha za umoja.
5) Umoja huu utatoa mchango kwa mwana umoja yeyote atakayefiwa au atakayekuwa anauguza mmojawapo wa ndugu wafuatao;
   a) Mama mzazi/Mama mlezi
   b) Baba mzazi/Baba mlezi
   c) Mke/Mume.
   d) Mtoto wa kumzaa/Kumlea ambaye atakuwa ameorodheshwa kwenye daftari la uanachama.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

e) Michango hiyo itolewe pale mgonjwa atakapolazwa Hospitali kwa zaidi ya siku kumi (10) au pale mgonjwa atakapolazimika kupewa rufaa kwa matibabu zaidi katika Hospitali za Rufaa.

f) Kiasi cha mchango kwa kila mtegemezi aliyeorodheshwa hapo juu na ambaye atakuwa ameorodheshwa kwenye daftari la uanachama katika umoja, iwapo atakuwa na ugonjwa au kifo, utaratibu utaamuliwa na wana umoja katika mkutano wa kamati ya kusaidiana na kitishwa na mkuu kupitia sera ya kusaidiana wakati wa shida.

g) Bila kuathili uhai wa umoja huu, umoja utazingatia kiasi maalumu cha kubaki kweneye mfuko/ Benki kwa ajili ya kuendesha shughuli za umoja pamoja na mambo ya dharura ya kiutawala ndani ya umoja huu.

6) Sherehe za kifamilia na zingine zitaamuliwa na Mkutano Mkuu wa umoja, na Kiasi cha mchango kwa kila Mwana umoja au mtegemezi aliyeorodheshwa hapo juu itaamuliwa na wana umoja katika mkutano mkuu

7) Michango kuhusu shere mbalimbali itaamuliwa na Mkutano mkuu wa Umoja na kusimamiwa na kanuni za kusaidiana wakati wa shida na raha:

## SEHEMU YA TANO

### *5.0 KAZI NA WAJIBU WA WATENDAJI*

5.1 Watendaji watano wa kamati tendaji watakuwa na wajibu kama ifuatavyo: -

### *5.2 MWENYEKITI*

Mwenyekiti wa kamati tendaji atakuwa na kazi na wajibu kama ifuatavyo: -

a) Kuitisha na kuendesha vikao vya kamati tendaji na mkutano mkuu.
b) Msemaji mkuu wa Umoja katika masuala ya utawala.
c) Kulinda na kusimamia katiba ya Umoja wakati wa kuitekeleza majukumu ya umoja.
d) Kutia saini katika fomu za mikataba kati ya Umoja na taasisi zingine.
e) Msimamizi mkuu wa shughuli za Umoja.
f) Mtia saini/lakili katika akaunti ya Umoja.
g) Ndiye mwakilishi na msemaji wa umoja katika taasisi zingine za ndani na nje ya nchi



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

### *6.3 : MWENYEKITI MSAIDIZI*

**atatekeleza Majukumu ya Mwenyekiti Mkuu pale asipokuwepo.**

### *6.4 KATIBU MTENDAJI*

Katibu mtendaji wa kamati tendaji ya Umoja atakuwa na kazi na wajibu kama ifuatavyo:

a) Mtendaji mkuu wa shughuli za Umoja.

b) Kuratibu shughuli za Umoja.

c) Kutunza kumbukumbu za vikao vya Umoja na wanaUmoja wenyewe.

d) Kuandaa na kutoa taarifa ya ujumla ya maendeleo ya shughuli za Umoja katika vikao vya umoja na wadau wa umoja huu.

e) Kutia saini katika akaunti ya Umoja

f) Kuandaa agenda za vikao akishirikiana na Mwenyekiti

### *6.5 KATIBU MSAIDIZI*

Atatekeleza Majukumu ya Katibu Mkuu pale atakapokosekana.

### *6.6 MTUNZA FEDHA*

Mtunza fedha wa Umoja atakuwa na kazi na wajibu kama ifuatavyo: -

1) Kupokea, kutunza na kulipa fedha za wana umoja.

2) Kuandaa na kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za wana umoja

3) Kuwafuatilia wanaodaiwa na Umoja huu.

4) Kutunza kumbukumbu za mahesabu ya fedha za Umoja.

5) Kutia saini katika akaunti ya Umoja.

6) Kuandaa makisio ya mapato na matumizi ya umoja kwa kila wa mwaka

7) Kuwa msimamizi mkuu wa mali za Umoja

8) Kubuni na kuibua vyanzo vya mapato

REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

# 7.0 SEHEMU YA SABA

## *7.1 SHUGHULI ZA UCHAGUZI*

## *7.2 UCHAGUZI WA WAJUMBE WA KAMATI TENDAJI.*

Wajumbe tano (5) wa kamati tendaji ambao ni Mwenyekiti, Mwenyekiti msaidizi, Katibu, Katibu msaidizi na Mtunza Fedha watachaguliwa na Mkutano mkuu. Itakapofika wakati wa kuajiri wataalamu katika nafasi hizi, utaratibu wa ajira utatumika kama ambavyo sera ya ajira ya umoja itafafanua upatikanaji wa wataalamu kwa nafasi husika.

## *7.3 MUDA WA UONGOZI*

i. Viongozi wa kuchaguliwa watakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu (3).
ii. Kiongozi ataruhusiwa kuwa madarakani kwa nafasi yake kwa vipindi vitatu vya uchaguzi, baada ya hapo kiongozi hata kama anasifa, atatakiwa kubadilishwa nafasi ya uongozi na si kurudia nafasi ile ya awali.
iii. Viongozi wa kuajiriwa/ watumishi watakuwa na mkataba wa ajira ambao utaandaliwa na umoja na kuongozwa na kanuni za ajira zitakazo undwa.

## *7.4 UCHAGUZI MKUU.*

Uchaguzi mkuu wa Umoja utafanyika kila baada ya muda wa viongozi wa kuchaguliwa kufikia ukomo wa kuwa madarakani ambapo ni baada ya miaka mitatu (3).

## *7.5 UCHAGUZI MDOGO*

Umoja huu utaitisha uchaguzi mdogo iwapo viongozi wa kuchaguliwa wa kamati tendaji mmoja wapo kati yao atafikia ukomo wa uongozi wa umoja kwa sababu moja wapo ya hizi zifuatazo: -

a) Kuhama.

b) Kufariki dunia.

c) Kufukuzwa uanaUmoja.

d) Kujiuzuru uanaUmoja.

e) Akiwa na sababu yoyote itakayo mfanya ashindwe kuendelea na uongozi wa umoja huu, uchaguzi mdogo utafanyika ili kujaza nafasi yake ndani ya siku Tisini (90).



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

### *7.6 KAMATI YA UCHAGUZI*

(1) Kutakuwa na Kamati ya Uchaguzi ambayo wajumbe wake watachaguliwa katika Mkutano Mkuu kwa ajili ya shughuli maalum ya uchaguzi husika kwa wakati huo.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Uchaguzi watakuwa watano na Miongoni Mwao watachagua Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi.

(3) Watasimamia Uchaguzi kuanzia wajumbe kuomba nafasi hadi kutangaza Matokeo baada ya kuridhiwa na kamati tendaji pamoja na Bodi ya wadhamini ambao katika uchaguzi wowote watakuwa waangalizi.

(4) Viongozi wakuu wa Umoja, (Kamati Tendaji) watapatikana kwa kuchaguliwa na wanaumoja katika Mkutano Mkuu wa Umoja kwa kura za siri.

(5) Baada ya kuchaguliwa viongozi wa Kamati Tendaji watatangazwa nas kujaza fomu za kukiri kusimamia umoja siku hiyo hiyo na wataanza kazi mara moja.

(6) Ikiwa kiongozi aliyechaguliwa atajiuzulu, kuondoka au kuondolewa madarakani kwa sababu yoyote ile, Mkutano Mkuu wa dharura utaitishwa ndani ya siku Tisini (90) ili kufanya uchaguzi wa kujaza nafasi iliyo wazi na anayechaguliwa atamalizia kipindi cha uongozi kilichobaki. Utekelezaji wa hili utategemea uwepo wa bajeti ya kufanya hivyo.

## SEHEMU YA NANE

### *8.0 MIKUTANO.*

### **8.1** USIMAMIZI WA UMOJA

Umoja huu kwa ujumla utasimamiwa na kuongozwa na vyombo vinne (4) ambavyo ni kamati Tendaji, kamati ya Uratibu, kamati ya usimamizi, pamoja na Mkutano mkuu.

### 8.2 KAMATI TENDAJI

a) Kamati tendaji ya Umoja itakuwa na wajumbe Tano (5) waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa mwaka ambao ni Mwenyekiti, Mwenyekiti msaidizi, Katibu, Katibu msaidizi na Mtunza Fedha.

b) Viongozi wa kamati hii wanaweza kuwa/kuitwa watumishi wa umoja ambao kwa mujibu wa katiba na matakwa ya wanachama wa umoja huu, yanaweza kufanyika maamzi ya kuajili watumishi wenye sifa kwa kila nafasi husika pale itakapo lazimika. Aidha sifa za watumishi hao zitaainishwa katika kanuni za ajira na Utumishi za umoja huu.

c) Bila kuathili sehemu ya 5.1 kwa mujibu wa katiba hii wajumbe hao kwa sasa watabaki kuwa wajumbe wa kamati Tendaji mpaka pale ambapo matakwa ya katiba yataruhusu vinginevyo.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

### 8.3 KAMATI YA URATIBU NA USIMAMIZI.

i. Kamati ya uratibu ya Umoja huu itaundwa na wajumbe wawakilishi wawili (2) kutoka kila Kanda ambao watakachaguliwa kutoka mikoa inayounda kanda husika yenye mamlaka za Umma zenye makatibu wa kamati ambao watathibitishwa na Mkutano Mkuu.

ii. Wajumbe hao wawakilishi toka kila Kanda wataunda kamati ya wajumbe kumi (10). Wajumbe wanaobakia, watakuwa wajumbe washauri wa kamati husika.

iii. Aidha kamati ya wajumbe 10 wa kamati ya uratibu na ushauri watawasilisha taarifa ya kazi zao kwa wajumbe wa kamati hii walio bakia kabla ya kuwasilisha taarifa yao katika mkutano mkuu.

### 8.4 MKUTANO MKUU.

Mkutano mkuu wa Umoja huu utajumuisha wanachama wote wa Umoja kutoka Mikoa yote pamoja na Halmashauri/ mamlaka za Umma za ndani ya Jamuhuri ya muungano wa Tanzania.

### 8.5 MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU.

a) Mkutano mkuu utakaa mara mbili (2) kwa mwaka
b) Kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa kamati tendaji
c) Kutoa maamuzi juu ya mapendekezo ya kumsimamisha uanachama wa mwanachama anayetuhumiwa kuwa na tabia mbaya, chanzo cha migogoro au anashindwa kutimiza matakwa ya katiba ya umoja.
d) Kutoa maamuzi ya kuyakubali au kuyakataa maombi ya wanachama wapya wanaotaka kujiunga katika Umoja huu.
e) Kuchagua wajumbe saba watakaounda Kamati Tendaji ya Umoja.
f) Kukitokea utata katika uendeshaji miongoni mwa wajumbe wa kamati tendaji, Mkutano Mkuu utabeba jukumu la kufanya mabadiliko yoyote yenye maslahi kwa Umoja wa "TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION".
g) Kuidhinisha kuingizwa au kufukuzwa kwa mwanachama katika Umoja huu.

### 8.6 MAJUKUMU YA KAMATI YA URATIBU NA USIMAMIZI

a) Kutoa ushauri wa utekeleaji majukumuya kila siku ya umoja huu
b) Kuwa washauri wa mwenendo wa wajumbe wa kamati ya utendaji ambao kwa upande mwingine wataweza kuitwa watumishi wa umoja pale ambapo itahitajika
c) Kufanya majukumu mengine ambayo mkutano mkuu utaagiza kufanya



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

### 8.7 MAJUKUMU YA KAMATI TENDAJI

(a) Itakuwa na mamlaka ya kusimamia na kuendesha shughuli za kila siku za Umoja.

(b) Kuandaa ajenda za Mkutano Mkuu na kuzisoma kwenye Mkutano husika.

(c) Kutekeleza maagizo ya Mkutano Mkuu.

(d) Kuandaa na kutoa taarifa ya maendeleo ya shughuli za Umoja

(e) Kuandaa ratiba ya mikutano yote ya Umoja kwa kila msimu wa mwaka

(f) Kuwajibika kwa Mkutano Mkuu.

(g) Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Umoja katika vikao vya Umoja.

### 8.8 MAJUKUMU YA KAMATI YA NIDHAM NA MAADILI

Kamati ya nidhamu itakuwa na kazi na majukumu kama ifuatavyo; -

1) Kumuonya mwana umoja ambaye anaonekana kuwa na tabia ambayo ni kinyume na kanuni na taratibu kwa mujibu wa katiba ya Umoja huu.
2) Kutoa mapendekezo ya kumsimamisha uanaUmoja mwanaUmoja ambaye amekuwa na tabia mbaya na sugu katika uvunjaji wa katiba ya Umoja na mapendekezo hayo yatawasilishwa kwa katibu wa kamati Tendaji ya Umoja ambaye atayaingiza katika ajenda za Mkutano Mkuu wa Umoja.

### 8.9 UENDESHAJI WA MIKUTANO

Bila kuathiri maelekezo yaliyomo katika katiba hii, mikutano ya Umoja huu itazingatia mambo yafuatayo;

1) Katika Umoja huu Mkutano halali ni lazima uhudhuriwe na nusu au zaidi ya wajumbe halali. Isipokuwa kwa Mkutano wa dharura, theluthi moja ya wajumbe wanaopaswa kuhudhuria Mkutano huo wakihudhuria, itaufanya Mkutano huo kuwa halali.
2) Mkutano Mkuu wa kawaida utaitwa kwa kutoa taarifa ya siku ishirini na moja (21), isipokuwa Mkutano Mkuu wa dharura utakuwa halali kwa kutoa taarifa ya siku kumi na nne (14).
3) Mkutano wa dharura wa kamati Tendaji ya Umoja unaweza kuitishwa na ukawa halali ikiwa nusu ya wajumbe halali wa kikao husika watahudhuria.
4) Mkutano wa dharura wa Umoja utaitishwa baada ya kupokea maoni kutoka theluthi moja ya wajumbe wa Mkutano Mkuu ambao wanaweza kuomba kwa maandishi kutaka uitishwe Mkutano Mkuu wa dharura. Maombi yanapaswa yaonyeshe agenda husika ya Mkutano huo.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

5) Katika uendeshaji wa mikutano ya Umoja, ikihitajika Mkutano kutoa maamuzi kwa kupiga kura, kura itakuwa ya siri za wanachama hai kwa mujibu wa katiba hii.

6) Mjumbe yeyote hatakuwa na haki ya kikatiba ya kuwakilishwa na mwana umoja Mwingine katika zoezi la upigaji wa kura.

7) Mkutano ulioahirishwa utaitishwa tena ndani ya muda wa siku sitini (60) au kwa kadiri itakavyoamuliwa na mamlaka husika.

## SEHEMU YA TISA

### *9 . 1 VYANZO VYA MAPATO VYA UMOJA*

Umoja huu utakuwa na mamlaka ya kupokea fedha kutoka katika vyanzo vifuatavyo: -

a) Malipo ya ada, kiingilio na hisa za wanachama.
b) Michango ya wanachama.
c) Faini mbalimbali za Umoja.
d) Mapato mengine kutoka shughuli mbalimbali au miradi ya Umoja (iwapo nitaanzishwa).
e) Misaada kutoka kwa wahisani mbalimbali.
f) Mauzo ya vitu/mali zitakazopatikana ndani ya miradi ya Umoja au kutoka kwa wahisani mbalimbali

### *9.2 UTUNZAJI WA FEDHA ZA UMOJA*

Fedha za umoja huu zitatunzwa Benki ambayo itakuwa imekubalika katika mkutano mkuu au kamati tendaji vinginevyo kama itakavyokuwa imeamuliwa na mkutano mkuu. Pia mkutano utapanga kiasi kidogo cha fedha anazostahili mtunza fedha kuifadhi mkononi kwa ajili ya shughuli za dharura zitakazojitokeza pamoja na shughuli za uendeshaji wa shughuli ndogo ndogo za kila siku za umoja.

### *9.3 MWAKA WA FEDHA*

Mwaka wa fedha wa umoja huu kwa mujibu wa katiba hii, utaanza mwezi Julai ya kila mwaka.

### *9.4 MATUMIZI YA FEDHA ZA UMOJA.*

Matumizi ya fedha za umoja huu yatafuata maamuzi ya mkutano mkuu wa wanachama na bajeti iliyopitishwa na mkutano mkuu. Aidha taarifa ya matumizi itatakiwa kuwasilishwa kwenye vikao husika kwa ajili ya kujiridhisha na uhalali wa matumizi husika

### *9.5 UTOAJI WA FEDHA BENKI.*

Kutakuwa na waweka saini wanne (4) katika kutoa fedha kwenye akaunti ya Umoja ambapo kundi la kwanza litakuwa na wajumbe wawili kutoka kwa kamati tendaji na kundi la pili itakuwa miongoni



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

mwa wajumbe. Aidha saini mbili (2) zitaruhusiwa kukubalika kutoa fedha benki ambapo mmoja atatoka kundi la kwanza na mmoja lazima atoke kundi la pili. Watia saini hao kutoka kundi la kamati tendaji watakuwa ni Mwenyekiti na Mtunza Fedha na ambapo kundi la pili ni Katibu pamoja na mjumbe atakayependekezwa na kamati tendaji pamoja na kuwasilishwa taarifa katika mkutano mkuu..

## SEHEMU YA KUMI

### *10. KAMATI MBALIMBALI*

i. Kutakuwa na Kamati mbalimbali kulingana na mahitaji ya Umoja, muundo na majukumu yataainishwa kwenye kanuni za Umoja.
ii. Kamati nyingine zitakuwa hazina wakati maalumu wa kukutana. Pale penye hitaji la kufanya hivyo watafanya hivyo. Pia kamati hizi zitaundwa na kamati tendaji kadiri ya mahitaji na kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kupitishwa.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

### *11. BODI YA WADHMINI*

a. Itaanzishwa Bodi ya wadhamini ya Umoja ambayo itakuwa MDHIBITI wa rasilimali za Umoja kwa niaba ya Umoja. Bodi itasajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Nchi.

b. Bodi ya wadhamini itakutana japo kwa mara moja kwa kila mwaka mmoja wa kalenda. Bodi itamteua mmojawapo wa Wajumbe wake kuwa Mwenyekiti wa Bodi. Wajumbe wa Bodi watachaguliwa na Mkutano Mkuu na hawatazidi watano au wasipungue watatu. Wajumbe wa Bodi ya wadhamini watakuwa katika madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na baadaye wanaweza kuchaguliwa tena.

c. Mtu anayestahili kuteuliwa kuingia katika bodi ya wadhamini lazima awe na sifa zifuatazo:-

i) Wataalamu wastaafu wa taaluma yoyote ambao watakuwa tayari kusaidia umoja kiuchumi pale inapobidi

ii) Kiongozi yoyote wa taasisi ambaye yupo katika utumishi ambaye atakubali kuwa mjumbe wa bodi

iii) Mwenyekiti wa umoja atakuwa mjumbe wa Bodi ya wadhamini.

iv) Awe mwenye umri usiopungua miaka 35 na usiozidi miaka 75.

D. Shughuli za Bodi ya wadhamini itakuwa:-

i) Kushauri namna ya kuimarisha umoja

ii) Kusaidia kutoa ushauri wa namna ya kuongeza mapato ya umoja



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

iii) Kusaidia kutoa ushauri wa kitaalamu

iv) Kudhibiti mali za Umoja kwa uaminifu wa Umoja

v) Kujadili/kupanga njia muafaka jinsi ya kuendeleza mali/utajiri wa Umoja.

vi) Kusimamia na kushauri namna ya kushughulikia mashitaka yote ya Umoja.

vii) Kufanya majukumu mengine ambayo kamati tendaji itaona inafaa bila kuathili katiba ya umoja.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

### *MIGOGORO NDANI YA UMOJA NA UTATUZI WAKE*

12. Iwapo itatokea hali ya kutoelewana miongoni mwa wana umoja kiasi cha kutishia usalama wa Umoja, Mwenyekiti atachukuwa hatua zifuatazo: -

a. Mwenyekiti atawasilisha shitaka husika kwa kamati ya nidhamu na maadili ambayo itakuwa na jukumu moja tu la kutafuta suluhu kwa ajili ya kuumaliza mgogoro.

b. Kamati hii itakuwa na kazi ya kuitisha kikao cha upatanishi ambapo wanachama wawili au zaidi watakaokuwa wanahusika na mgogoro, watapewa taarifa ya mwaliko wa kuhudhuria kikao husika.

c. Iwapo juhudi za Kamati ya nidhamu na na maadili zitashindwa kuzaa matunda, kamati hiyo itaandaa taarifa na kuiwasilisha kwa Mwenyekiti wa Umoja ambaye atampatia katibu kwa ajili ya kuingiza katika ajenda za Mkutano Mkuu. ***Hii itakuwa ni hatua ya juu sana na itafikiwa baada ya hatua za awali kushindwa kufikia suluhu.***

   i. Iwapo Mwenyekiti na Katibu watajadiliana na kubaini kuwa mgogoro ni mgumu na kwamba utahitaji kuujadili kwa muda mrefu kabla haujapatiwa ufumbuzi, viongozi hao wanaweza kuomba kuitisha Mkutano Mkuu Maalum wa Umoja ambao utakuwa na agenda moja tu.

   ii. Iwapo Mkutano Mkuu utagundua kuwa mwana umoja ndio chanzo cha mgogoro, Mkutano Mkuu utakuwa na madaraka ya kumchukulia hatua ya kutoa adhabu kwa kupanga kiasi cha faini atakayotakiwa kulipa ndani ya muda utakaopangwa na Mkutano Mkuu husika au kadiri mkutano mkuu utakavyo wweza kukasimu madaraka kwa kamati tendaji au vinginevyo..

   iii. Iwapo mhusika atakaidi kulipa adhabu hiyo, Mkutano Mkuu utakuwa na haki ya kumfukuza uanachama au kumpeleka katika vyombo vya kisheria.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

iv. Pamoja na kuwa na uwezo wa kamati ya kushughulikia mgogoro uliojitokeza, kamati hii itakuwa na mamalaka ya kushughulikia mgogoro unaohusu mwanachama

v. Lakini ili kuimarisha umoja Mkutano Mkuu unaweza kuunda kamati ya wajumbe wasiopungua 5 (tano) na wasiozidi 10 (kumi) na kuipa jukumu la kuzuia na kutatua migogoro.

vi. Kamati ya kuzuia migogoro na kusuluhisha migogoro ikishaundwa itakaa madrakani kwa kipindi cha kusuluhisha mgogoro husika.

vii. Migogoro itakayoshindwa kutatuliwa ndani ya umoja itafikishwa Ofisi ya Msajili wa Jumuya au kwenye vyombo ya maamuzi ya Nchi. ***Hatua hii ni ya mwisho kabisa na kwa mujibu wa katiba hii, umoja hauweki kipaumbele kuifikia.***

## SEHEMU YA KUMI NA TATU

### *13.0 MAREKEBISHO*

Ni kawaida kufanya marekebisho kwa lengo la kuboresha jambo lolote wakati wowote. Kwa hiyo marekebisho yanakubaliwa na Katiba hii kwa utaratibu utakaowekwa na katiba hii na kukubaliwa na Mkutano mkuu. Aidha marekebisho hayo yawe ni kwa maslahi ya umoja na yapate ridhaa na wanaumoja wasiopungua theluthi tatu ya wanachama wa umoja huu.

### *13.2 IDHINI YA MAREKEBISHO YA KATIBA*

Hakuna kitu chochote katika katiba hii kitakachorekebishwa, kubadilishwa, kufutwa au · kutenguliwa, isipokuwa kwa maazimio yatakayo pitishwa na Mkutano mkuu wa Umoja ambao utakuwa umeitishwa kwa ajili hiyo. Mkutano huu utaitishwa iwapo robo tatu ya wajumbe wataona kuwa kuna haja ya kufanya mabadiliko hayo kwa maslahi ya Umoja.

## SEHEMU YA 14.

### *KUVUNJIKA KWA UMOJA*

Umoja huu utaweza kuvunjika iwapo kutatokea mambo yafuatayo: -

a) Iwapo Mkutano Mkuu utatoa uamuzi wa kuvunja Umoja kutokana na kuwepo na sababu zozote ambazo itaonekana ni jambo la busara kuvunja Umoja.



REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

b) Ikitokea mamlaka za kiutawala katika nchi zikaagiza kuvunjika kwa vikundi vinavyofanya shughuli kama za Umoja huu wa “TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION”.

c) Kufilisika kwa umoja kiasi cha kushindwa kujiendesha

d) Iwapo itatokea hali kama hiyo ya kuvunjika kwa Umoja, mali za Umoja zitagawanywa sawa kwa wanachama wote wa umoja wa “TANZANIA COMMITTEE CLERK UNION” ambao hawatakuwa wanadaiwa na Umoja. Mwanachama atayekuwa anadaiwa, atapewa mgawo baada ya kukatwa kiasi anachodaiwa. Iwapo deni litakuwa kubwa kuliko kiasi cha mgawo, mdaiwa atawajibika kulipa kiasi kinachozidi mgawo. Kama atashindwa, atapelekwa mbele ya vyombo vya kisheria

## HITIMISHO

Katiba hii imesomwa, kujadiliwa na kupitishwa na wanachama wote.

REGISTRAR OF SOCIETIES
29 NOV 2024
P.O. Box 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS